**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

## KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
## YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII

# TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI, 2022 HADI JANUARI, 2023

[Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]

**FEBRUARI, 2023**

**YALIYOMO**


YALIYOMO ..... i

SEHEMU YA KWANZA ..... 1

**1.0** MAELEZO YA JUMLA ..... 1

- 1.1 Utangulizi ..... 1
- 1.2 Muundo wa Taarifa ..... 1
- 1.3 Msingi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ..... 2
- 1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika ..... 3

**SEHEMU YA PILI ..... 4**

2.0 **SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA ..... 4**

- 2.1 Maelezo ya Shughuli ..... 4
  - 2.1.1 Kupokea Taarifa za utekelezaji wa Maazimio ..... 4
  - 2.1.2 Kushughulikia Bajeti ..... 4
  - 2.1.3 Kufuatilia Utekelezaji wa Shughuli zinazotekelezwa na Wizara ..... 5
  - 2.1.4 Yaliyobainika katika Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ..... 6
  - 2.1.5 Yaliyobainika wakati wa ufuatiliaji wa Sekta ..... 8
    - 2.1.5.1 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Maliasili na Utalii ..... 9
    - 2.1.5.2 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ..... 27
- 2.2 Semina kwa Wajumbe wa Kamati ..... 37

**SEHEMU YA TATU ..... 39**

**3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ..... 39**

**3.1 Maoni ya Jumla ..... 39**

- 3.1.1 Wizara ya Maliasili na Utalii ..... 39
- 3.1.2 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ..... 40
- 3.2 MAPENDEKEZO ..... 40
  - 3.2.1 Maboresho ya eneo la hifadhi ya ngorongoro ..... 40
  - 3.2.2 Urejeshaji wa Asilimia 30 ya Makusanyo (retention) ..... 41
  - 3.2.3 Kulijengea uwezo Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) ..... 41
  - 3.2.4 Changamoto za Wanyamapori Wakali na Waharibifu ..... 42
  - 3.2.5 Kutungwa kwa Sheria ya Uendeshaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) ..... 42
  - 3.2.6 Hali ya Utalii Nchini ..... 43
  - 3.2.7 Changamoto za Taasisi za Utafiti za (TAFORI & TAWIRI) ..... 43
  - 3.2.8 Usimamizi wa Rasilimali za Misitu Nchini ..... 44
  - 3.2.9 Kutokuwepo kwa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba kila Wilaya Nchini ..... 44
  - 3.2.10 Taasisi na Mashirika ya Umma kutolipa Kodi ya Pango la Ardhi ..... 44
  - 3.2.11 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Mawaziri 8 wa Kisekta katika Kutatua Migogoro ya Vijiji 975 Nchini ..... 45
  - 3.2.12 Kuhuisha Sera mbalimbali zilizopitwa na wakati ..... 45
  - 3.2.13 Kuanzishwa kwa Mamlaka ya kusimamia Sekta ya Nyumba Nchini (Real Estate Regulatory Authority - RERA) ..... 46
  - 3.2.14 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ..... 46
  - 3.2.15 Maboresho ya Mfumo Unganishi wa Kumbukumbu za Taarifa za Ardhi (ILMIS) ..... 47
  - 3.2.16 Utendaji wa Hotel na Loji za Serikali zilizobinafsishwa. ..... 47
  - 3.2.17 Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi ..... 48

**SEHEMU YA NNE ..... 49**

**4.0 HITIMISHO NA KUFUNGA HOJA ..... 49**

- 4.1 Hitimisho ..... 49
- 4.2 HOJA ..... 50

## TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI 2022 HADI JANUARI, 2023

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa Kipindi cha Kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023. Taarifa hii imejikita katika kuelezea shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kipindi cha mwaka mmoja.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imeundwa na sehemu kuu nne kama ifuatavyo: -

i) Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, mbinu na njia zilizotumika pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja;

ii) Sehemu ya pili inafafanua shughuli zilizotekelezwa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto zilizojitokeza;

iii) Sehemu ya tatu inatoa maoni ya jumla na mapendekezo ili kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi, na

iv) Sehemu ya nne inatoa hitimisho na kutoa hoja kwa ajili ya Bunge kuweza kujadili na kufanya maamuzi.

## 1.3 Msingi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati unatokana na Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo inaeleza kuwa lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi wake. Aidha Ibara ya 63(2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya Wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kifungu cha 6(6) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ina wajibu wa kufanya masuala mbalimbali yaliyoanishwa katika Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambayo ni: -

a) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na
d) Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Janauari January, 2022 hadi Februari, 2023 Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo: -

i) Kupokea na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Wizara hizo pamoja na taasisi zake.
ii) Kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara inazozisimamia;
iii) Kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2022/2023 za Wizara inazozisimamia.
iv) Kujadili taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba,2022);
v) Kufuatilia Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya Mwaka ya Kamati iliyowasilishwa Mwezi Februari, 2022

## 1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 142 ambayo pamoja na mambo mengine inataka kubainisha njia au mbinu zilizotumika. Njia kuu zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati ni zifuatazo: -

i) Kufanya vikao na Wizara inazozisimamia kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo na Taasisi zake;

ii) Kufanya ziara kwa lengo la kujionea utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake na kuzilinganisha na taarifa iliyochambuliwa na Kamati;

iii) Kufanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali, ikiwemo taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa Mwaka 2021/2022 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

iv) Kushiriki mafunzo, semina na warsha mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Wizara, Mashirika ya Umma, Taasisi Binafsi, Asasi za Kiraia na wadau wengine katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii; na

v) Kufanya majumuisho ya mambo yaliyobainika kwenye vikao wakati wa majadiliano ili kuorodhesha mambo makuu ya kutolewa maoni na ushauri.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kutumia mbinu hizi tofauti ni kuwawezesha wajumbe wa Kamati kujielimisha kwa kiwango cha kutosha katika nyanja ambazo wanawajibika kuzisimamia na kuishauri Serikali.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

### 2.1 Maelezo ya Shughuli

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hii inasimamia shughuli za Umma zinazotekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii ambapo inasimamia sekta kuu zifuatazo: -

(a) Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

(b) Sekta ya Maliasili na Utalii

**Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha masharti ya Kifungu cha 7(1) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge yanazingatiwa, Kamati ilipanga na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

#### 2.1.1 Kupokea Taarifa za utekelezaji wa Maazimio

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kupokea taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023. Lengo la kupokea taarifa hizi lilikuwa ni kufuatilia iwapo Serikali imezingatia Maazimo ya Bunge na kama imezingatia ni kwa kiasi gani yametekelezwa katika kuleta ustawi wa jamii.

#### 2.1.2 Kushughulikia Bajeti

**Mheshimwa Spika,** Kamati ilitekeleza jukumu hili la kuchambua na kupitia bajeti za Wizara zote mbili na taasisi zake. Jukumu hili lilitekelezwa ikiwa ni kutimiza takwa la Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu mapendekezo ya Bajeti ya Wizara zote mbili iliwasilishwa Bungeni wakati wa vikao vya Mkutano wa saba wa Bunge.

### 2.1.3 Kufuatilia Utekelezaji wa Shughuli zinazotekelezwa na Wizara

**Mheshimiwa Spika,** fasili ya 7(1)(d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, inazitaka Kamati za Kisekta kufanya ufuatiliaji wa shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Kwa kuzingatia sharti hilo la kikanuni, Kamati imetekeleza shughuli mbalimbali za ufuatiliaji wa shughuli zinazotekelezwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maliasili na Utalii. Shughuli hizo zinajumuisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti, kwa dhumuni la kujiridhisha kuwa malengo yaliyokusudiwa na bajeti hizo yanafikiwa. Shughuli hii ilitekelezwa kwa kupokea taarifa za utekelezaji wa bajeti kutoka Wizara zote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilifanya ufuatiliaji wa Utendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa kupokea taarifa mbalimbali za utendaji katika vikao mbalimbali vya Kamati. Lengo la shughuli hii ni kujiridhisha kwamba dhima ya ustawi wa wananchi kupitia sekta zinazosimamiwa na Wizara hizi inafikiwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilifanya ziara za ufuatiliaji kwa lengo la kujiridhisha na tija inayopatikana katika miradi na program zinazotekelezwa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati. Kutokana na Ziara hizo Kamati iliweza kuwianisha taarifa zinazotolewa na Serikali kuhusu tija na mafanikio na hali halisi iliyopo kwenye maeneo husika. Kamati ilitembelea Pori la Akiba Swagaswaga – Dodoma kuona hali ya Pori, Mvomero-Morogoro kuona namna wananchi wanavyopambana na wanyama wakali na waharibifu, Eneo la Msomera –Tanga kuona maendeleo na hatua zilizofikiwa katika kuhamisha kwa hiari wananchi toka eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro na Hifadhi ya Taifa Mkomazi kuona miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 na NHC Dar Es Salaam kuona utekelezaji wa miradi ya Morocco Square na Kawe 711.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya uchambuzi wa bajeti za Wizara kwa Mwaka 2022/2023 Kamati ilitembelea na kukagua miradi Nane (8) iliyotekelezwa na wizara hizi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Tolea la Juni, 2020. Aidha, Kamati pia ilipata fursa ya kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 kwa kipindi cha nusu mwaka Julai-Disemba.

### 2.1.4 Yaliyobainika katika Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa kupitia taarifa za utekelezaji wa maazimio, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa maazimio ulikuwa katika hatua tofauti ambapo kulikuwa na maazimio yaliyotekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha na kuna maazimio yaliyotekelezwa kwa sehemu na mengine yalikuwa kwenye hatua za awali za utekelezwaji kama ifuatavyo.

#### (i) Sekta ya Maliasili na Utalii

**Mheshimiwa Spika**, sekta hii ilikuwa na maazimio sita (6) ambapo yaliyotekelezwa kwa kiwango cha kujiridhisha katika ngazi ya sekta ni maazimio mawili. Azimio la kwanza lililotekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha katika ngazi ya sekta ni agizo la kupandisha hadhi Wakala wa Misitu (TFS) ambapo Kamati ilijulishwa kuwa andiko liko kwenye ngazi za maamuzi. Kamati inaamini kuwa hatua hii pia itakamilika kwa haraka ili kunusuru misitu ya nchi yetu iliyo katika hatari ya kutoweka kutokana na kukosa usimamizi mzuri katika ngazi zote.

**Mheshimiwa Spika,** Azimio la pili lililotekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha katika ngazi ya sekta, ni Azimio la kulipandisha Bonde la Mto Kilombero kuwa Pori la Akiba ambapo andiko lipo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kamati inaamini kuwa utekelezaji wa azimio hili

utahakikisha usalama wa bonde muhimu la Kilombero ambalo mradi mkubwa wa Bwawa la Mwalimu Nyerere unategemea maji kwa zaidi ya **asilimia 60**.

**Mheshimiwa Spika,** yapo maazimio 4 yaliyotekelezwa kwa sehemu. Mfano utekelezaji wa azimio la kutungwa kwa Sheria ya Uendeshaji wa Mamlaka ya Wanyapori (TAWA) bado upo kwenye ngazi ya wizara ambapo andiko bado linaboreshwa. Kutokamilika kwa andiko hili mapema kunaendelea kuikosesha nguvu ya kisheria mamlaka hii na hivyo kukosa tija iliyokusudiwa;

**Mheshimiwa Spika**, Maazimio ambayo hayakutekelezwa ni pamoja na Azimio la kulijengea uwezo Shirika la Hifadhi za Taifa ambapo shirika linaendelea kutekeleza majukumu yake chini ya kiwango kutokana na ufinyu wa bajeti.

**(ii) Sekta ya Adhi**

**Mheshimiwa Spika,** katika sekta hii, kulikuwa na jumla ya maazimio 6 ambapo hakuna maazimio yaliyotekelezwa kwa ukamilifu. Aidha, maazimio yaliyotekelezwa kwa sehemu ni maazimio 5. Miongoni mwa maazimio hayo ni azimio la kuitaka Wizara kupitia NHC kukamilisha miradi ambayo imechukua muda mrefu. Kamati imebaini kuwa miradi hii bado iko katika hatua tofauti za utekelezaji. Mfano, Mradi wa Kawe 711 umesimama kwa miaka 4 na unaweza kuisababisha Serikali kuingia hasara kubwa baada ya Mkandarasi wa mradi huu kuidai Serikali fidia ya zaidi ya **Shilingi Bilioni 47** baada ya mradi kusimama kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika**, Maazimio ambayo hayakutekelezwa ni pamoja na azimio la kuitaka Serikali kuhakikisha makampuni yote yaliyopewa kazi ya kurasimisha makazi katika jiji la Dodoma na hayajakamilisha kazi hiyo kwa zaidi ya mwaka mmoja yatimize wajibu wao wa kisheria.

**Mheshimiwa Spika**, Maazimio yaliyofikiwa na Bunge yalilenga kuongeza tija katika shughuli za Wizara hizi ili kuweza kufikiwa kwa ustawi wa wananchi. Hata hivyo, kasi ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge bado si ya kuridhisha, hivyo Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika kutekeleza maagizo ya Bunge lako.

### 2.1.5 Yaliyobainika wakati wa ufuatiliaji wa Sekta

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Januari, 2022 hadi Februari, 2023, Kamati ilipokea na kujadili taarifa 36 ambapo taarifa 19 ni za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na taarifa 17 ni za Wizara ya Maliasili na Utalii. Lengo la kupokea na kujadili Taarifa hizi ni kuiwezesha Kamati kulisaidia Bunge kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imelipa Bunge mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii ya Taarifa inalenga kuonesha uchambuzi wa kina wa yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Kamati ambapo matokeo ya uchambuzi yanajumuisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti za Wizara kwa kipindi cha nusu mwaka pamoja na taarifa za utendaji wa Wizara, mafanikio na changamoto kwa kila sekta kama ifuatavyo: -

**(i) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba),2022.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kuchambua utekelezaji wa bajeti za Wizara zote mbili kwa kipindi cha nusu Mwaka kuanzia Julai hadi Disemba,2022. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwepo na changamoto mbalimbali kama vile fedha kutotolewa kwa wakati, fedha kutolewa chini ya kiwango na kufanya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuwa chini ya kiwango.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa mjadala wa kuhitimisha bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Waziri

wa Fedha na Mipango aliahidi kuongeza bajeti ya maendeleo ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kiasi cha **Shilingi Bilioni nne (4).** Wakati wa uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya nusu mwaka ya 2022/2023, Kamati ilibaini kuwa fedha hiyo ya nyongeza ya **Shilingi Bilioni nne** haikuonekana katika vitabu vya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kama ilivyoahidiwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka ufafanuzi wa hali hii na kufahamishwa kuwa Wizara inaendelea kufanyia kazi suala hili kwa kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili nyongeza hiyo izingatiwe na kuingizwa katika bajeti ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** ni matumaini ya Kamati kwamba fedha hizo zitatolewa kikamilifu na kwa wakati ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Kamati yangu itaendelea kufatilia kwa karibu suala hili ambalo Kimsingi linahusu utekelezaji wa ahadi ya Serikali Bungeni.

**(ii) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Wizara na Taasisi zake**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa utendaji wa Wizara zinazosimamiwa na Kamati unajumuisha mafanikio na changamoto kwa kila sekta kama ifuatavyo: -

**2.1.5.1 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Maliasili na Utalii**

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Maliasili na Utalii imekuwa na mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi na ukuaji wa uchumi. Uchambuzi wa taarifa uliofanywa na Kamati, umewezesha kubaini mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya sekta ya maliasili na utalii kwenye miradi na taasisi zake kama ifuatavyo;

a) **Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) - Moshi**

M**heshimiwa Spika**, Chuo hiki kina jukumu kubwa la kutoa mafunzo ya teknolojia ya viwanda vya misitu kwa ngazi ya cheti na diploma. Aidha, pamoja na mafunzo haya, chuo kinatoa mafunzo ya muda mfupi ya uvunaji wa miti, uchakataji wa magogo, usimamizi wa viwanda vya misitu na upangaji wa madaraja ya ubora wa mbao na nguzo. Pia chuo kinatoa huduma za ushauri na utafiti kuhusu usimamizi wa viwanda vya misitu na uongezaji wa thamani wa bidhaa zitokanazo na viwanda vya misitu na uvunaji wa misitu.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na malengo mazuri ya uanzishwaji wa chuo hiki na mafanikio yaliyofikiwa, Kamati ilibaini kuwa Chuo kinakabiliwa na changamoto kubwa ya Ufinyu wa bajeti ya ruzuku inayoidhinishwa kwa chuo ukilinganisha na mahitaji halisi ya chuo ambapo, mahitaji halisi ya ruzuku ni **shilingi 1,050,425,000** kwa mwaka lakini chuo kimeidhinishwa **shilingi 255,425,550** sawa na **asilimia 24 tu** na Upungufu wa watumishi hasa walimu wa fani za uhandisi, tehama, viwanda vya misitu na uchumi. Hali hiyo imepelekea chuo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

b) **Programu ya kuongeza Mnyororo wa Thamani ya Mazao ya Misitu Kibiashara (FORVAC)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa program inalenga kuongeza faida za kiuchumi, kijamii na kimazingira zinazotokana na misitu ya asili pamoja na kupunguza uharibifu wa misitu kwa kupitia mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu. Aidha, Kamati ilifahamishwa juu ya hatua mbalimbali zilizofikiwa ikiwa pamoja na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi vijiji 34;

kuwezesha vijiji kuwa na mashine jongea (mobile sawmill) na za teknolojia ya kisasa ya kuongeza ufanisi, ubora na mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu; kuwajengea uwezo wanavikundi kwa kuwanunulia vifaa vya kuanzisha uzalishaji pamoja na kuwaunganisha na mnyororo wa masoko.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na mradi huu, bado utekelezaji wake ulikumbana na changamoto za uvamizi wa baadhi ya maeneo ya misitu kutokana na shughuli za kila siku za kibinadamu; mioto inayowaka msituni na kuathiri uoto uliopo na bioanuai muhimu kwa maisha ya watu; utengaji wa maeneo madogo kwa ajili ya Hifadhi za Ufugaji Nyuki kutokana na uelewa mdogo wa jamii kuhusu uanzishwaji wa Hifadhi za Nyuki; na ufinyu wa bajeti ya utekelezaji zimekuwa kikwazo katika utekelezaji wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kuhusu uhifadhi wa misitu na upandaji miti kibiashara maeneo mbalimbali nchini, Kamati inaona bado kuna umuhimu wa Serikali kutoa elimu ya kutosha na endelevu kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa misitu kwa lengo la kuongeza thamani ya mazao ya misitu, kuongeza pato la Serikali pamoja na ustawi wa wananchi wake.

**c) Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro (1959) iliweka msingi wa kuendesha Mamlaka hii kama eneo la matumizi mseto.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake wa kuona namna bora ya kuhifadhi eneo la Ngorongoro ambalo kwa miaka mingi ardhi yake imetumika kwa matumizi mseto (Multiple Land use) na kuja na

suluhisho la kuhamisha wakazi wanaoishi ndani ya hifadhi hii kwa hiyari.

**Mheshimwa Spika**, Serikali ilifanya maamuzi ya kuhamisha wenyeji hao kwa lengo la kupunguza ongezeko la watu na mifugo, makazi ya kudumu na holela, shughuli za binadamu zinazotishia kupoteza hadhi ya Hifadhi hiyo kama eneo la urithi wa dunia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa Wizara imebainisha maeneo mbadala ya Handeni - Tanga na Kitwai - Manyara kwa ajili ya makazi ya wananchi wanaoendelea kuhama toka hifadhini. Katika Mpango huu hadi kufikia Novemba, 2022 Serikali imefanikiwa kuhamisha jumla ya kaya 489 zenye watu 2,629 na mifugo 14,094. Aidha, jumla ya kaya 1,524 zenye watu 8,715 na mifugo 32,842 zimejiandikisha kuhama kwa hiari.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhika na uratibu mzuri wa zoezi hili ambalo ni la hiari na linalozingatia haki za binadamu ambapo Serikali inawapa huduma zote muhimu kwa kuwapatia chakula, nyumba, shule ya msingi, Sekondari na Bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum, miundombinu ya maji, miundombinu ya mawasiliano, umeme, majosho 3, na vitalu vya malisho.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango huu, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na; upotoshwaji unaofanywa na baadhi ya Taasisi zisizo za kiserikali pamoja na baadhi ya watu waliopo ndani na nje ya nchi; na watu wasiokuwa na sifa za kuhamishwa kutaka kutumia fursa hii ili wahamishwe kinyume na taratibu.

**Mheshimiwa Spika**, kwakuwa zoezi hili limeonyesha muitiko mkubwa toka kwa wakazi wa Ngorongoro kutokana na uhamasishaji uliofanywa na Serikali ni rai ya Kamati kuwa Serikali itoe fedha za kutosha na kwa wakati ili kukamilisha zoezi hili.

**d) Mradi wa kuongeza idadi ya Faru na Mbwa Mwitu katika Hifadhi ya Mkomazi**

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la kuanzisha hifadhi ni kuimarisha uhifadhi wa eneo hili pamoja na rasilimali zilizomo, na kukuza utalii kwa faida ya kizazi kilichopo na kijacho. Hifadhi hii ina aina mbalimbali za wanyama wakiwemo wanyama walio hatarini kutoweka duniani kama Faru na Mbwa Mwitu hivyo kupelekea kuanzisha miradi yenye lengo la kuongeza idadi ya wanyama hawa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuhusu mafanikio ya mradi huu ikiwa pamoja na kuongezeka kwa wanyama hawa ambapo mradi wa faru katika mradi wa Kisima una Faru 30, Mbula 6. Aidha Jumla ya mbwa mwitu 237 wamezaliwa na 202 kati yao wameachiwa katika maeneo mbalimbali ndani ya Mkomazi kuanza maisha huru katika maeneo yao ya asili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza mafanikio haya na kuitaka Serikali kuendelea kusimamia mradi huu ili kuhakikisha kuwa wanyama hawa ambao wako kwenye hatari ya kutoweka wanatunzwa na kuongezeka.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado zipo changamoto zinazoathiri kuongezeka kwa haraka kwa idadi ya wanyama hawa ambazo ni; miradi kutokuwa na chanzo cha uhakika cha maji kwa matumizi ya wanyama na watumishi; uchakavu wa mitambo na ukosefu wa fedha za kufanyia matengenezo ya mashine na magari ya mradi; na tishio la faru kuzaliana wenyewe kwa wenyewe. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ihakikishe jamii ya Faru na Mbwa Mwitu waliobaki wanawekewa mikakati madhubuti ya kutunzwa na kulindwa ili isipotee ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanalindwa dhidi ya maradhi na ujangili.

e) **Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI)**

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) ilianzishwa kwa lengo la kufanya tafiti, kusimamia, kuratibu na kutoa taarifa za tafiti mbalimbali zinazohusu wanyapori pamoja na kushirikiana na taasisi mbalimbali zilizo nje na ndani ya nchi kufanya tafiti za wanyamapori na kuishauri Serikali, mamlaka za usimamizi wa wanyamapori na Watanzania kwa ujumla kuhusu uhifadhi endelevu wa wanayamapori.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa baadhi ya mafanikio ya kiuhifadhi yaliyotokana na shughuli za utafiti wa wanyamapori nchini ikiwa ni pamoja na kupata ushindi wa kwanza kwenye Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) kwa ugunduzi wa nishati ya mkaa mbadala "*briquettes*" kwa kutumia mimea vamizi; kutoa elimu ya kukabiliana na wanyama wakali na waharibifu; kuratibu ongezeko la idadi ya wanyama walioko kwenye hatari ya kutoweka mfano duma, faru weusi na mbwa mwitu; ugunduzi wa aina mpya ya kipepeo aitwae Charaxes mtuiae katika bonde la Kihansi; na hatimiliki mbili (two patents) za ugunduzi wa mimea miwili iliyotumika kwa tiba ya kuotesha nywele au kuzuia nywele kutoka (activity for hair loss prevention and growth) na uweo wa kuboresha rangi ya ngozi (activity for skin lightening).

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi kubwa inayofanywa na TAWIRI, inakabiliwa na changamoto zifuatazo: upungufu wa ofisi jambo linaloifanya taasisi iingie gharama za kukodi/kupangisha; uchakavu wa miundombinu; upungufu wa vitendea kazi; na Uhaba wa vifaa vya maabara. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iendelee kutatua changamoto hizi ili Taasisi hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuleta ustawi wa wananchi ambalo ni lengo kuu la serikali kwa mujibu

wa Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya Mwaka 1977.

**f) Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala ulianzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha uwepo wa usimamizi madhubuti na wenye ufanisi na tija ya rasilimali za misitu na nyuki pamoja na kuongeza ubora na thamani ya kifedha katika kutoa huduma kwa umma.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza serikali kupitia Wakala kwa kuhakikisha kuwa inahamasisha ushiriki wa jamii kwenye shughuli za uhifadhi. Aidha wakala umeimarisha mfumo wa kuzuia ujangili wa maliasili za nchi kwa kutoa mafunzo ya utayari katika Vyuo vya Pasiansi na Mlele; umefanya mapitio ya mipaka na kubadilisha mipaka ya misitu 27 kama njia ya kutatua migogoro ya wananchi na kupelekea utatuzi wa migogoro katika vijiji 204 kutoka mikoa ya Tabora, Geita, Dodoma, Morogoro, Pwani, Tanga na Mara; na wakala kwa kushirikiana na JWTZ ilikamilisha jukumu la kusafisha eneo la Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere kufikia kontua 184 kutoka usawa wa bahari.

**Mheshimiwa spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, TFS inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazotokana na uhitaji mkubwa wa mazao ya misitu mfano; utegemezi mkubwa wa misitu kwa ajili ya nishati ya kupikia hususani mkaa na kuni kumesababisha uvunaji holela wa misitu kwa kiasi kikubwa na kuzorotesha juhudi za Wakala; uvamizi wa hifadhi kwa ajili ya makazi, mifugo, kilimo au madini; kukinzana kwa sera na vipaumbele vya kisekta mfano mifugo, kilimo na madini; Matukio ya moto na Upungufu wa watumishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza kuwa Serikali iweke utaratibu mzuri wa mawasiliano kati ya sekta

zinazohusika na uchimbaji wa madini, makazi, mifugona kilimo na kuhakikisha kuwa shughuli hizi zinazingatia uhifadhi wa misitu.

**g) Kukabiliana na Wanyama Wakali na Waharibifu hususani Tembo na Mamba.**

**Mheshimiwa Spika**, Migongano baina ya binadamu na wanyamapori ni moja ya changamoto zinazokabili uhifadhi wa wanyamapori nchini, Kamati ilijulishwa kuwa katika kutekeleza sera, sheria, Kanuni na kwa kuzingatia ongezeko kubwa la matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara iliandaa na inaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa kusimamia utatuzi wa migongano baina ya binadamu na wanyamapori (2020-2024).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kutekeleza Mkakati huu ikiwa ni pamoja na kuendesha doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, kutoa elimu kwa wananchi juu ya mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na kufuatilia mwenendo wa migongano, na ujenzi wa vituo 16 vya kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo ya kipaumbele hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio haya, Kamati ilibaini kuwa zipo changamoto zinazoikabili Wizara katika kukabiliana na Wanyama wakali na waharibifu ambazo ni upungufu wa Askari wa Uhifadhi ambapo kwa sasa taasisi za uhifadhi wa wanyamapori zina upungufu wa jumla ya askari wahifadhi 1,687 (TANAPA 466, NCAA 290 na TAWA 931); upungufu wa magari, helikopta na pikipiki zitakazotumika na Askari Wahifadhi na VGS/mgambo katika doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu; na ukosefu wa maji na chakula ndani ya

maeneo yaliyohifadhiwa kulingana na mahitaji na kusababisha mtawanyiko wa wanyamapori kutoka nje ya maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya kutafuta maji na chakula.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua na kuthamini jitihada mbalimbali ambazo Serikali imekuwa ikichukua katika kukabiliana na changamoto hizi. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuishirikisha Kamati mara kwa mara katika masuala yanayohusu uhifadhi, fursa zinazoiwezesha Kamati kutoa ushauri wake katika jitihada za kukabiliana na changamoto mbalimbali za uhifadhi.

**h) Hali ya Utalii Nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania imejaliwa kuwa na vivutio vingi vya utalii kutokana na utajiri wa maliasili kama vile wanyamapori, misitu, bahari, maziwa, fukwe nzuri na utamaduni wa Watanzania unaojumuisha jamii zenye tamaduni mbalimbali. Vivutio hivi vimeifanya sekta ya utalii kuendelea kuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa kwa kuchangia zaidi ya **asilimia 25** ya mauzo yote ya nje na kutoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja **1,600,000** kabla ya UVIKO 19.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada mbalimbali zilizofanywa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Sekta binafsi katika kukuza, kuendeleza na kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii hususani, kwa kutumia program maalumu ya *Tanzania-The Royal Tour* baada ya sekta hii kukumbwa na changamoto za mlipuko wa UVIKO-19.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na jitihada hizo, Kamati ilibaini mafanikio yaliyopatikana ikiwa pamoja na kuongezeka kwa Idadi ya Watalii wa Kimataifa, kutoka **Watalii 922,692** Mwaka 2021 hadi kufikia **Watalii**

**1,454,920** Mwaka 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 57.7**. Aidha, Idadi ya watalii wa ndani wameongezeka kutoka **788,933** mwaka 2021 hadi **2, 363,260** mwaka 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 199.5.**

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio mengine ni kuongezeka kwa Idadi ya wakala wa biashara za utalii waliosajiliwa na kupatiwa leseni wameongezeka kutoka wakala 1,869 mwaka 2018/2019 hadi kufikia wakala 5128 mwaka 2021/2022 sawa na **asilimia 174.4**. Katika kipindi hicho, maduhuli yaliongezeka kutoka Shilingi **Bilioni 5.5** kwa **Mwaka 2018/2019** hadi **Shilingi Bilioni 7.1** Mwaka wa Fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kukuza utalii, ni rai ya Kamati kuwa Serikali iweke mkakati madhubuti wa kuhakikisha kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassani – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Programu ya ***Tanzania- The Royal Tour*** inakuwa endelevu kwa kuweka mazingira mazuri yatakayohakikisha watalii wanaendelea kuja na kufurahia utalii Tanzania na kuongeza mapato.

**i) Changamoto za kuzibwa kwa Shoroba katika Hifadhi za Taifa.**

**Mheshimiwa Spika**, Maeneo ya hifadhi na mifumo ikolojia ya wanyamapori yanaunganishwa na shoroba ambazo huruhusu wanyamapori kuhama kutoka hifadhi au eneo moja kwenda nyingine kwa malengo mbalimbali ikiwemo kujihami, kuzaliana, maeneo ya mtawanyiko na maeneo muhimu kwa ajili ya kupata chakula na maji wakati wa msimu kiangazi wa mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi nchini, hususan Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID) kupitia mradi wa

RTI – Tuhifadhi Maliasili kuweza kufanya tathmini na kubainisha shoroba 61 za wanyamapori nchini na kuandaa Mpango kazi wa vipaumbele wa kuongoa shoroba hizo na kuandaa mwongozo wa utekelezaji wa mpango kazi huo.

**Mheshimiwa Spika**, kuziba kwa shoroba hizi kumepelekea changamoto nyingi hususani migongano baina ya binadamu na wanyamapori inayosababishwa na Wananchi wanaoendesha shughuli zao za kijamiii na kiuchumi katika maeneo ya shoroba ambapo wanakabiliwa na athari za kujeruhiwa; kuuawa; mazao kuharibiwa na mifugo kuuawa na hivyo kuongeza kiwango cha umaskini kwa wananchi; na wanyamapori kushindwa kubadilishana vinasaba (genetic exchange) na hivyo kusababisha kupotea kwa vizazi kwa baadhi ya wanyamapori ambao hawaruhusu inbreed.

**Mheshimiwa Spika**, ni wakati sasa wa Serikali kuweka alama za kudumu kwenye maeneo yaliyoanishwa kama shoroba ili kudhibiti uvamizi wa shughuli za kibinadamu.

**j) Hali ya Sekta ya Malikale na Mchango wake katika kuimarisha Utalii Nchini.**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta hii ni kati ya Sekta muhimu zinazochangia katika uhifadhi wa urithi wa Taifa na mazingira, maendeleo ya kiuchumi, kitamaduni na kijamii.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kujadili na kuchambua taarifa hii, mbali na mafanikio katika Sekta hii bado kwa kiasi kikubwa, shughuli za utalii Tanzania zimeendelea kutegemea zaidi vivutio vya urithi wa asili, hususan, hifadhi za wanyamapori na Mlima Kilimanjaro. Ikilinganishwa na nchi nyingine duniani.

Aidha, Sekta ya Utalii Tanzania inakabiliwa na changamoto ya wigo mdogo wa mazao ya utalii ikiwemo

suala zima la utalii wa kihistoria. Hali hii husababisha mtalii kukaa nchini kwa muda mfupi na pengine kutorudi tena baada ya kuwa ameona utalii wa vivutio vya asili, hususani, wanyamapori ambao pia wanapatikana katika nchi nyingine. Vilevile Sekta hii inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti jambo linalokwamisha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine ni Ushiriki mdogo wa serikali za mitaa katika uhifadhi wa malikale. Hii inachochewa na muundo wa TAMISEMI kutojumuisha usimamizi wa shughuli za malikale kwenye ngazi za Mikoa na Halmashauri; migogoro ya mipaka na Shughuli za kibinadamu katika maeneo ya malikale; na upungufu wa watumishi na vitendea kazi hasa wanaohusika na usimamizi na uendelezaji wa malikale na uhaba magari.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Malikale ni kati ya sekta muhimu zinazochangia katika uhifadhi wa urithi wa Taifa, mazingira, maendeleo ya kiuchumi, kiutamaduni na kijamii ni vema Wizara ikaimarisha ushirikiano na Idara ya Mipango miji hasa katika ngazi ya Halmashauri ili kuhakikisha maeneo haya hayapotei au kutumika vinginevyo.

**k) Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mpango huu, Wizara ya Maliasili na Utalii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 90.2** sawa na **asilimia 6.9** ya fedha yote. Mpango kazi uliopitishwa na Wizara ulianisha maeneo makuu matano kwa ajili ya utekelezaji, ambayo ni kuziwezesha Taasisi za Wizara (TANAPA, TAWA, NCAA, TFS na NMT) zilizoathirika zaidi kutokana na mlipuko wa Uviko-19 kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kuimarisha masoko

na utangazaji utalii, kuimarisha mazingira ya biashara ya utalii kwa kuzingatia viwango vya afya na usalama vya kitaifa na kimataifa, kuimarisha sekta binafsi kwa kuwajengea uwezo wa kukabiliana na janga la UVIKO-19 na kuimarisha mifumo ya kidigitali ya takwimu za utalii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2022 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 89.2** sawa **na asilimia 98.86** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizotumika ni **Shilingi Bilioni 64** sawa na **asilimia 72** ya fedha zilizopokelewa. Aidha, kiasi cha **Shilingi Bilioni 25.2** zilikwa katika hatua tofauti za malipo**.** Kamati imeona kuna tija ya fedha zilizotengwa kuimarisha miundombinu ili kuimarisha sekta ya uhifadhi na utalii.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi wa taarifa hii Kamati ilihoji sababu za kuchelewa kutekelezwa kwa miradi hii licha ya kupewa fedha zote ambapo ilielezwa kuwa ni kutokana na hali mbaya ya hewa inayosababishwa na mvua za msimu, baadhi ya zabuni kurudiwa kutokana na kupanda kwa gharama na kuchelewa kwa ununuzi wa mitambo ikiwemo magreda, boti na magari maalum ambapo GPSA hawakuweza kufanikisha manunuzi kutokana na taratibu zilizopo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na uchambuzi wa utekelezaji wa miradi hii, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea miradi inayotekelezwa katika hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ambapo Kamati iliridhika na utekelezaji wa mradi unaotekelezwa katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro unaogharimu jumla ya **Shilingi Milioni 798.** Aidha, miradi inayotekelezwa katika Hifadhi ya Mkomazi ambayo inagharimu **Shilingi Bilion 4** haikuonekana kulingana na thamani ya fedha

iliyotumika, na utekelezaji wa miradi umechukua muda mrefu licha ya kupatiwa fedha zote kwa wakati.

**l) Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tanzania Wildlife Management Authority - TAWA)**

**Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tanzania Wildlife Management Authority - TAWA) ilianzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 8 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 na kutangazwa kwa amri (Order) ya Serikali iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 135 la tarehe 09 Mei 2014, pamoja na marekebisho yaliyochapishwa katika gazeti la Serikali Na. 20 la tarehe 23 Januari 2015. TAWA kwa kuchukua majukumu ya kiutendaji ya Idara ya Wanyamapori kuhusu usimamizi wa rasilimali ya wanyamapori nje ya Hifadhi za Taifa na Hifadhi ya Ngorongoro.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu. Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazokabili Mamlaka ambazo ni pamoja na;

- upungufu mkubwa wa Watumishi hasa askari wa uhifadhi ambapo kuna watumishi 1,855 kati ya 3,600 wanaohitajika licha ya kuwa na eneo kubwa la usimamizi jambo linalochangia ongezeko la ujangili na uvamizi wa mifugo katika hifadhi.
- Matukio ya wanyamapori kuvamia na kusababisha madhara kwa maisha na mali za wananchi yameendea kuongezeka kutoka matukio 1,706 mwaka 2020/21 hadi matukio 2,304 mwaka 2021/2022.

- Kuongezeka kwa matukio ya wanyamapori kuuawa na majangili wanaotumia mitego ya waya hususan kwenye mfumo ikolojia wa Serengeti jambo ambalo ni hatari kwani inaua wanyama wengi na hata wale ambao hawakuwa wamekusudiwa.
- Uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Mathalan, Pori Tengefu la Kilombero ambalo ni chanzo kikuu cha maji ya mto Rufiji yanayotegemewa kuzalisha umeme katika Bwawa la Mwl. Nyerere kwa mfano katika mwaka wa fedha 2021/22 pekee jumla ya mifugo 9,196 ilikamatwa katika pori tengefu Kilombero jambo linalokwamisha juhudi za Serikali katika kukamilisha Mradi mkubwa kama huu.
- Kuwepo Kwa kampeni za kupinga uwindaji wa kitalii zinazofanywa kupitia Asasi zisizo za Kiserikali kwa madai ya kutetea haki za Wanyama unaathiri tasnia ya uwindaji na mapato kwa ujumla

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Pori Tengefu wa Kilomero, Serikali ichukue hatua za haraka za kuwaondoa wananchi katika Pori hili ambalo ni chanzo kikuu cha maji ya mto Rufiji yanayotegemewa kuzalisha umeme katika Bwawa la Mwl. Nyerere.

**m) Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI)**

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) ina jukumu la kufanya, kusimamia, na kuratibu tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi ya teknolojia bora na uendelezaji wa misitu nchini. Aidha, mwanzoni mwa mwaka 2019, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ilihamishia shughuli za utafiti wa Ufugaji nyuki TAFORI kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI).

**Mheshimiwa Spika** Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Taasisi hii katika masuala ya utafiti. Hata hivyo Kamati ilibaini kuwa Taasisi hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo za ufinyu wa Bajeti ambapo kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2021/22, Taasisi imekuwa ikipata kiasi cha **Shilingi Milioni 279** kwa ajili ya matumizi mengineyo wakati mahitaji halisi ni **Shilingi Bilion 2.7.**

**Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine upungufu wa watumishi na kutoidhinishwa kwa muundo mpya wa Taasisi ambapo maombi yaliwasilishwa mamlaka husika tangu 2019, muundo huo unaopendekeza kuanzisha kwa kurugenzi mpya ya Utafiti wa Nyuki baada ya kuhamisha masuala yote ya utafiti wa ufugaji nyuki kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI); Aidha Taasisi inakabiliwa na changamoto ya uchakavu na upungufu wa miundombinu. Pia Taaisisi hii inakabiliwa changamoto ya madeni makubwa ambapo hadi kufikia June, 2022, Taasisi ilikuwa inadaiwa jumla ya **Shilingi Milioni 757,778,860.00** hali hii inachangiwa kwa kuwa na bajeti ndogo ambayo haikidhi mahitaji halisi ya Taasisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona kuwa bado Taasisi hii haijapewa uzito inaostahili kulingana na umuhimu wa majukumu yake.

**n) Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inalipongeza Shirika la Hifadhi za Taifa kwa kazi linazofanya katika Sekta ya Utalii ambapo Shirika limeweza kupata tuzo mbalimbali zikiwemo Tuzo ya Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa Hifadhi Bora Barani Afrika kwa miaka minne mfululizo (2019, 2020, 2021 na 2022). Tuzo hii imetolewa na “World Travel Awards na Hifadhi ya Taifa Serengeti ilitangazwa na

gazeti maarufu duniani la “Forbes” kuwa moja ya vivutio bora duniani vya utalii kutembelea kwa mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa zinazokabili hifadhi zetu ikiwa pamoja na Mtawanyiko wa Hifadhi za Taifa (Remoteness and distribution of National Parks) kwa ujumla wake unasababisha gharama kubwa za uendeshaji; Upungufu wa rasilimali za kutosha kuendesha maeneo ya uhifadhi hususan hifadhi za kusini, magharibi na mashariki ambazo uzalishaji haukidhi mahitaji ya uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine ni pamoja na Shirika kuongezewa idadi ya Hifadhi za Taifa kutoka hifadhi 16 hadi 22, lakini bado Shirika linatumia bajeti ya hifadhi 16 tangu Mwaka 2019 jambo linalopelekea shirika kutotekeleza majukumu yake kwa ukamilifu; Uingizwaji wa mifugo katika Hifadhi za Taifa kinyume cha Sheria; Ujangili wa wanyama na rasilimali nyinginezo ndani ya hifadhi husababisha gharama ambazo shirika lingetumia kwa ajili ya uwekezaji katika miundombinu; Migogoro kati ya binadamu na wanyama wakali na waharibifu; Mimea vamizi katika hifadhi za Taifa inayoharibu ubora wa makazi ya wanyamapori na malisho.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia hali ya kifedha ya Shirika kwa sasa na taratibu zilizopo za ukusanyaji wa maduhuli sanjari na hali ya upatikanaji wa fedha kutoka hazina ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali iweke utaratibu wa TANAPA kupata fedha za kujiendesha kwa wakati na kwa ukamilifu kwa kuwa mfumo uliopo sasa unafanya TANAPA kuwa na mazingira magumu ya biashara ya utalii na kukabiliana majanga pindi yanapotokea mfano janga la moto katika Mlima Kilimajaro

**o) Utendaji wa Hotel na Loji za Serikali zilizobinafsishwa**.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma nchini ulianza kutekelezwa Mwaka 1992, baada ya Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1969 kufanyiwa marekebisho. Mabadiliko hayo yalilenga kuiwezesha Sekta Binafsi kushiriki katika umiliki, uwekezaji, na uendelezaji wa Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mpango huu, Serikali ilibinafsisha Hotel na Loji 23, ambapo kati ya hizo, Loji 4 zipo ndani ya Hifadhi ambazo ni loji za Seronera na Lobo (Hifadhi ya Serengeti), Mikumi Wildlife Lodge (Mikumi) na Ngorongoro Wildlife Lodge katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupokea na kujadili Taarifa hii, Kamati ilijulishwa kuwa Hoteli 10 zimewekezwa kulingana na masharti ya Mikataba ya mauziano, Loji na Hotel 6 uwekezaji uliofanyika haulingani na matakwa ya Mikataba ya Mauziano, wawekezaji wametekeleza chini ya viwango vilivyokubalika na Hotel 7 zipo kwenye hatua mbalimbali za ukarabati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupokea taarifa hii, Kamati ilibaini kuwa Serikali imekuwa ikichelewa kuchukua hatua stahiki pindi Mwekezaji anapokiuka masharti ya mkataba na kusababisha Serikali kukosa Mapato na kuharibu taswira ya nchi, Mathalani kampuni ya Hotels and Loji Limited anayomiliki loji za Ngorongoro Wildlife, Seronera Wildlife na Lobo Wildlife zilizopo ndani ya hifadhi na Hotel za Lake Manyara Hotel na Mafia amekiuka masharti ya Mkataba tangu alipouziwa Mwaka 2002.

**Mheshimiwa Spika**, Lake Manyara Hotel ni hotel iliyopo katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro lakini haihesabiki kuwa miongoni mwa hotel zilizopo hifadhini, na hivyo kupelekea uwekezaji wake kuwa tofauti na hotel

zilipo Hifadhini, ni maoni ya Kamati, kuwa Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kuiongeza Lake Manyara Hotel kuwa moja ya hotel zilizopo ndani ya hifadhi kwa lengo la kuongeza mapato na kupunguza tatizo la malazi hifadhini.

### 2.1.5.2 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Mheshimiwa Spika**, ardhi imeendelea kuwa miongoni mwa rasilimali za msingi katika ujenzi wa uchumi wa Taifa na ustawi wa wananchi wake. Ardhi imekuwa muhimu katika kuziwezesha sekta nyingine kuzalisha kikamilifu hususan sekta za uzalishaji kama vile kilimo, mifugo, uvuvi pamoja na maeneo ya ardhi kwa ajili ya madini na ujenzi wa viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, ardhi ikiboreshwa itapunguza migogoro ya ardhi kwa kiasi kikubwa. Kamati imebaini mafanikio na changamoto katika sekta ya ardhi kwa miradi na taasisi zifuatazo: -

**a) Utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa na Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi ambayo ina lengo la kuwezesha usimamizi madhubuti na wenye mpangilio unaofaa wa matumizi ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu umefanikiwa katika kutekeleza shughuli mbalimbali kama uandaaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya wilaya ambapo tume imefanikiwa kuwezesha uandaaji wa Matumizi ya Ardhi wa Wilaya ya Nzega ambayo ni moja ya wilaya zilizopitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi (EACOP); Utatuzi wa migogoro ya ardhi ya muda mrefu katika vijiji 10 vya wilaya 4 za Chalinze (2),Nzega (3), Sumbawanga (3) na Nkasi (2) iliyotokana na mipaka ya kiutawala na kuwezesha mamlaka za upangaji kutoa vyeti vya ardhi na vijiji na hati za Hakimiliki za Kimila.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilfahamishwa kuwa mradi unakumbana na changamoto mbalimbali katika utekelezaji ambazo baadhi yake ni kuongezeka kwa muda wa uaandaji wa

mipango ya matumizi ya ardhi na gharama kutokana na uwepo wa migogoro ya ardhi inayotokana na mipaka ya kiutawala na matumizi katika maeneo mbalimbali ya vijiji; kutokuwa na mawasiliano na uratibu wa pamoja na Wizara za kisekta wakati wa uanzishwaji wa vijiji vipya kutoka vijiji mama bila kupima mipaka ya kiutawala, ufinyu wa bajeti na uhaba wa vitendea kazi hasa magari na vifaa vya upimaji (GPS, RTK) hali inayosababisha baadhi ya shughuli za uwandani kutokamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huu, ni wazi kuwa Tume kwa ujumla itatekeleza miradi yake kwa uchache kutokana na bajeti ndogo inayotengwa mwaka kwa mwaka hasa bajeti ya maendeleo. Ni maoni ya Kamati kuwa, ili Serikali iweze kufanikiwa katika kutekeleza sehemu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2020- 2025 wa kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi nchini kwa asilimia 50 ya vijiji 12,319 vilivyopo nchini ifikapo mwaka 2025. Ni muda sasa wa Serikali kuongeza bajeti ya Tume.

**b) Chuo cha Ardhi Tabora**

**Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Ardhi Tabora kilianzishwa kwa lengo la kuzalisha wataalamu wa sekta ya ardhi ngazi ya mafundi sanifu (Technicians) kutokana na kuongezeka kwa uhitaji wao nchini. Katika kutekeleza majukumu yake, chuo kimefanikiwa pamoja na mambo mengine katika urasimishaji wa maeneo katika Mitaa mbalimbali nchini kwa kutumia fedha za mkopo shilingi 644,590,300.00 zilizotolewa na Wizara ya Ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa katika utekelezaji wa majukumu yake, chuo hiki kinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa watumishi ambapo chuo kina jumla ya watumishi 35 na mahitaji halisi ni watumishi 55; baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati kutokana na kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha za maendeleo.; na ufinyu wa bajeti umesababisha chuo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi ya msingi ya chuo ya kuzalisha wataalamu wa sekta ya ardhi, bado chuo kina hitaji kutengewa bajeti ya kutosha ili kutekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa.

c) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za NHC ya Morocco Square na Kawe 711

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba katika maeneo mbalimbali nchini ni sehemu ya majukumu ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). Moja ya miradi inayotekelezwa na Shirika ni ujenzi wa miradi ya Morocco square na Kawe 711.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa miradi hii umechukua muda mrefu kukamilika kutokana na kusimama kwa muda mrefu; kupanda kwa vifaa vya ujenzi; na madai ya fidia yatokanayo na kusimama kwa mradi ambapo katika Mradi wa Kawe 711 mkandarasi anadai fidia ya **shilingi Bilioni 47.4** Aidha, Kamati ilifahamishwa kuwa serikali iko katika hatua ya mazungumzo na mkandarasi kuhusiana na madai hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona kuna haja ya NHC kuharakisha kukamilisha mazungumzo na mkandarasi ili kuokoa fedha ambayo inaendelea kuongezeka kutokana na mazungumzo kutofika mwisho.

**d)** Makusanyo ya Maduhuli katika Sekta ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na majukumu mengine inalo jukumu la kukusanya maduhuli ya Serikali yatokanayo na sekta ya ardhi kwa kuzingatia Sera, kanuni na sheria mbalimbali. Katika taarifa hii, Kamati ilibani kuwa Wizara imefanikiwa kukusanya mapato kwa **asilimia 36.1** ya lengo kufikia Desemba, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeona kuwa ukusanyaji wa maduhuli katika sekta hii si wa kuridhisha ambapo Wizara ilieleza kuwa halii hii imesababishwa na uwepo wa malimbikizo ya muda mrefu ya kodi yapatayo **Bilioni 65** kutoka kwenye taasisi na mashirika ya umma; mwamko mdogo wa wananchi kulipa gharama za umilikishaji; na kodi ya pango kutolipwa kwa wakati. Ni vema

Serikali ikabuni njia mbalimbali za kuhamisha kulipa madeni hayo kama vile kufanya matangazo na kutuma jumbe kwa njia za simu.

e) **Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi nchini.**

**Mheshimiwa Spika**, programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi Nchini (KKK) ni programu ya miaka 10 inayotekelezwa na Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini ambapo utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika mwaka 2028/2029. Katika utekelezaji wa miradi hii, Serikali imefanikiwa kutambua vipande vya ardhi 28,069 katika halmashauri za Misungwi, Meru, Karatu, Loliondo na Monduli umefanyika na uwekaji kumbukumbu za vipande vya ardhi nchini kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji; na kutekeleza programu katika miradi ya kimkakati (EACOP) ambapo maeneo yanazunguka bomba la mafuta katika halmashauri ya Misenyi – Kagera na Geita jumla ya viwanja 2,011 vimepangwa;

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa, Programu hii imekabiliwa na changamoto kama mwamko mdogo wa wananchi kuchangia gharama za upangaji na upimaji ardhi; ushiriki wa watumishi wa ardhi kwenye zoezi la anuani za makazi limeathiri kasi ya utekelezaji wa programu; na baadhi ya wananchi kutokuwa tayari kutoa maeneo ya kutwaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kupanga kupima na kumilikisha ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huu, kamati inaona ipo haja ya Serikali kuanzisha mfuko wa KKK kama ulivyo mfuko wa Maji ambapo mfuko huo utatumika kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi nchini hasa vijiji miji na kupunguza au kuondoa makazi holela na kupanua wigo wa walipa kodi.

f) **Kamati ya Mawaziri Nane (8) wa Kisekta kushughulikia Migogoro ya Ardhi Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hii iliundwa kufuatia kuwepo kwa migogoro mbalimbali ya matumizi ya ardhi nchini ambayo

inawahusisha wananchi wenyewe au Serikali na wananchi katika maeneo mbalimbali nchini. Kamati hii ilifanya uchambuzi wa vijiji/mitaa vyenye migogoro ya matumizi ya ardhi katika mikoa yote ya Tanzania Bara ambapo, kwa mujibu wa taarifa ya Kamati hiyo, zoezi hili limebainisha jumla ya vijiji/mitaa 975 vyenye migogoro.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupokea taarifa hii, Kamati ilijulishwa kuwa Kamati ya Mawaziri Nane (8) iliwasilisha taarifa yake kwenye Baraza la Mawaziri ambalo lilielekeza pamoja na mambo mengine kumega maeneo ya Hifadhi, Mapori Tengefu, Mashamba, Ranchi, Misitu ya Hifadhi, kulipa fidia kwa wananchi wanaoondolewa katika maeneo yaliyobainishwa, kufanya marejeo ya matangazo ya serikali GN yaliyoanzisha maeneo hayo na kuwaondoa wanachi walivamia maeneo yaliyobainishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii inayolenga kutatua migogoro ya ardhi nchini. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa katika utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri, kumekuwa na changamoto zifuatazo: -

- Utekelezaji wa maamuzi haya kutokuwa shirikishi katika ngazi za chini; na
- Kutokuwepo kwa Utaratibu Maalumu (Mechanisms) wa ufuatiliaji wa maagizo ya yanayotolewa na Mawaziri 8 kwa viongozi wa mikoa na wilaya.
- Kamati ya Mawaziri 8 kutokufika kwenye maeneo ya migogoro (uwandani) ili kuona uhalisia na kutatua migogoro na badala yake kufika kwenye ofisi za mkoa na Wilaya na kutoa maagizo.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Mawaziri wa kisekta usipozingatia ushirikishwaji na kuweka utaratibu maalumu (mechanism) wa ufuatiliaji, ufanisi ulikusudiwa hautafanikiwa hivyo kutokuendana na utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala (CCM) Ibara ya 73 (g) na ambayo inalenga kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi nchini, kuchochea ukuaji wa uchumi na kuimarisha usalama wa wananchi na mali zao.

**g) Utendaji wa Mfuko wa Fidia ya Ardhi**

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Fidia ya Ardhi ni chombo kilichoanzishwa chini ya kifungu cha 173 cha Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 kwa madhumuni ya kulipa fidia kwa mtu aliyepoteza haki au maslahi katika ardhi kutokana na kutwaliwa kwa ardhi yake kupisha shughuli zinazofanywa na Serikali au taasisi ya Umma.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kuchambua taarifa hii, Kamati ilifahamishwa kuwa mfuko huu umefanikiwa kutoa jumla ya **Shilingi 654,000,000** kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi 123 katika jiji la Dodoma. Aidha, mfuko umefanikiwa kuandaa mwongozo wa kusimamia mfuko wa fidia ya ardhi (Operational Manual for Managing Land Compensation Fund) wa mwaka 2016 ambao utausaidia mfuko kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi

**Mheshimiwa Spika**, mfuko huu unakabiliwa na changamoto kubwa ambapo taasisi zinazowajibika kulipa fidia zimekuwa na utaratibu wa kutenga fedha na kulipa fidia bila kupitisha fedha kwenye mfuko jambo ambalo linasababisha mfuko tukotekeleza majukumu yake ya msingi na hivyo kupunguza ufanisi uliotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,** ni rai ya Kamati kuwa, Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuhakikisha kuwa taasisi zote zinazotakiwa kupitisha fedha za fidia kwenye mfuko huu zinafanya hivyo kama sheria inavyotaka ili kuuwezesha mfuko kutekeleza majukumu yake na tija iliyokusudiwa inapatikana.

**h) Usimikaji wa Mfumo wa ILMIS katika Jiji la Dodoma**

**Mheshimiwa Spika**, Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi (ILMIS) umeanzishwa kwa lengo la kuboresha utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za ardhi pamoja na kuondoa ugumu wa kupata taarifa sahihi kwa wakati, kuongeza mapato pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa watumishi wa sekta ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** usimikaji wa mfumo huu katika Jiji la Dodoma umeweza kutoa Hatimiliki za kielekitroniki 11,126**.** Wizara imekamilisha kazi ya kuchambua, kupiga picha (scanning) na kuingiza kwenye mfumo michoro ya Mipangomiji yenye jumla ya viwanja 510,000 na Ramani za Upimaji zenye jumla ya viwanja 323,736 katika jiji la Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na usimikaji wa mfumo huu muhimu kwa ajili ya kutoa hati kwa haraka na kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi katika Jiji la Dodoma. Hata hivyo Kamati imebaini kuwa kumekuwa na ucheleweshwaji wa upatikanaji wa hati miliki kinyume na malengo ya usimikaji wa mfumo huu. Hivyo ni Dhahiri kuwa mfumo huu unahitaji maboresho makubwa ili ile tija iliyokusudiwa ipatikane na iweze kwenda sambamba na utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi ibara ya 74 (b) inasisisitiza uwekwaji wa mfumo unganishi wa kielekitroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za ardhi katika mikoa yote na wilaya zote nchini.

**i) Baraza la Taifa la Wapima Ardhi**

**Mheshimiwa Spika**, Baraza la Taifa la Wapima lina jukumu la kuhakikisha kuwa taaluma pamoja na wataalamu wa fani ya upimaji ardhi wanafanyakazi kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria husika.

**Mheshimiwa Spika**, Baraza linakabiliwa na changamoto mbalimbali kama Uhaba wa rasilimali fedha na watu kwa ajili ya kuendesha shughuli zake; Upungufu wa vitendea kazi hali inayopunguza tija iliyokusudiwa; na Mapungufu katika Sheria ya Upimaji na Ramani Sura ya 390 ambayo vifungu vingi vimepitwa na wakati inalinyima Baraza nguvu ya kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, maendeleo ya sekta ya ardhi yanategemewa kwa kiwango kikubwa kuchangiwa na wataalamu wa kada mbalimbali ndani ya sekta hii. Aidha, upungufu wa wataalamu na vitendea kazi katika sekta hii kunazorotesha ufanisi katika sekta ya ardhi.

**j) Uendelezaji wa Mashamba Makubwa ya Uwekezaji yaliyotelekezwa nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa umilikishaji na ubatilishaji wa ardhi iliyopangwa kwa ajili ya uwekezaji hufanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na mamlaka zingine za uwekezaji kwa kuzingatia sheria na taratibu husika. Zoezi hili ni endelevu ambapo katika kutekeleza haya Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Taasisi zingine zinazosimamia masuala ya uwekezaji na wawekezaji zimekuwa zikiendesha zoezi la kukagua na kuwakumbusha wamiliki wa mashamba kuhakikisha yanaendelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, zoezi hili linakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni baadhi ya wamiliki wa mashamba kutozingatia mikataba ya makabidhiano ya ardhi; baadhi ya wananchi kuvamia mashamba ya uwekezaji kwa kisingizio cha fidia; baadhi ya mashamba yaliyobatilishwa kutosimamiwa vyema kwenye ugawaji hasa katika ngazi ya Halmashauri. Hali hii inaongeza migogoro isiyo ya lazima.

**Mheshimiwa Spika,** jukumu la kusimamia na kuendeleza mashamba makubwa ni la wamiliki au wawekezaji wa mashamba. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ifanye uhakiki na usimamizi wa mara kwa mara ili kuhakikisha matumizi ya mashamba yanazingatia sheria na ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima.

**k) Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika Eneo la Msomera – Handeni – Tanga**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa kuhamisha makazi kwa wenyeji waishio ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kwa hiari ambapo una lengo la kuboresha maisha yao na kuimarisha uhifadhi wa mazingira, utalii na malikale katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza mradi huu**,** Serikali imefanikiwa katika mambo yafuatayo: Wizara kwa kushirikiana na

Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na wadau wengine kuandaa mwongozo wa uhamishaji makazi katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; kuandaa Mpango wa matumizi ya ardhi katika eneo la Msomera; kufanya uthamini na kuandaa majedwali ya fidia kwa wakazi wanaohama kwa hiari kutoka katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; na kuandaa hati za haki miliki za wakazi katika eneo la upangaji la Msomera.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo utekelezaji wa mpango huu unachangamoto ya uwepo wa GN iliyoanzisha Mapori Tengefu ya Handeni na Kitwai ambayo yamependekezwa kuwa makazi kwa wakazi wanaohamia toka Ngorongoro kwa hiari. Hali hii imesababisha ugumu katika kuwezesha mipango ya matumizi ya ardhi kupitishwa na mamlaka za upangaji ikiwemo Halmashauri za vijiji; na Uwepo wa Hati miliki za Kimila 21 kwenye eneo la upangaji la Msomera ambapo hati hizi zinahitaji kufutwa.

**Mheshimiwa Spika**, mpango huu ni moja ya mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wa Rais wa awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao unalenga kuinusuru Hifadhi ya Ngorongoro ambayo imekuwa kwenye hatari ya kutoweka. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iharakishe kufuta GN iliyoanzisha Mapori Tengefu ya Handeni na Kitwai ili kukamilisha zoezi la kupanga matumizi ya ardhi.

**l) Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa (International Boundaries)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa unalenga kutatua migogoro ya mipaka, kuboresha na kuimarisha mipaka kati ya Tanzania na nchi inazopakana nazo katika nchi kavu na mipaka iliyopo majini (Bahari, Mito na Maziwa).

**Mheshimiwa Spika**, katika kupitia taarifa hii, Kamati imebaini kuwa Serikali imefanikiwa kwa hatua tofauti tofauti kufanya zoezi la kuboresha na kuimarisha mipaka hii ya kimataifa kwa kushirikiana na nchi zinazohusika.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mradi huu, bado mradi unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile kukosekana kwa miundombinu ya barabara katika maeneo ya mipakani kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi na kurahisha zoezi la uimarishaji wa mipaka; uharibifu wa alama za mipaka kunakotokana na fikra potofu kwamba maeneo hayo yana vito vya thamani pamoja na utafutaji wa vyuma chakavu; upungufu wa wataalamu na vitendea kazi kwa ajili ya uimarishaji mipaka ndani ya maji; baadhi ya alama za asili zilizopo kwenye itifaki ya mpaka kutokuwepo ardhini mfano Mto Mwibu kati ya mpaka wa Tanzania na Burundi; na kupishana kwa upatikanaji wa fedha kwa mujibu wa makubaliano ya vikao kati ya nchi na nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kuwa Serikali ione umuhimu wa kutatua changamoto zilizopo ikiwa ni pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya kusomesha wataalam wa uimarishaji mipaka ndani ya maji**.**

**m) Uanzishwaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii ililenga kufahamu maendeleo ya uanzishwaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ambayo kwa kiasi kikubwa yamekuwa yakipunguza mlundikano wa mashauri yahusuyo ardhi katika ngazi za wilaya.

**Mheshimiwa Spika**, katika kupitia taarifa hii, Kamati imebaini kuwa Serikali imefanikiwa kuanzisha mabaraza mawili (**2**) ambayo ni Kishapu na Bahi katika kipindi cha mwaka mmoja Aidha, maeneo kwa ajili ya ofisi za mabaraza katika wilaya kumi (**10**) yamepatikana pamoja na wajumbe wa mabaraza hayo.

**Mheshimiwa Spika,** uanzishwaji wa mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika kila wilaya nchini ni jambo kubwa na muhimu kwa ustawi wa jamii kwani inawasaidia wananchi kupata huduma kwa karibu, na gharama nafuu na kwa haraka. Ni maoni ya Kamati kuona Serikali ione umuhimu wa kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya uanzishwaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika kila wilaya nchini.

## 2.2 Semina kwa Wajumbe wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati, wajumbe walipata fursa ya kushiriki katika semina mbalimbali ambazo zililenga kuwajengea uwezo baadhi ya semina hizo ni zifuatazo: -

**a) Semina Kuhusu Mwongozo wa Uwekezaji wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania.**

**Mheshimiwa Spika,** Semina hii iliandaliwa na kutolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kupitia semina hii wajumbe waliweza kupata uelewa wa kutosha kuhusu hatua za uwekezaji katika Hifadhi za Taifa ambazo zinahusisha maombi ya uwekezaji, usanifu wa miradi, utekelezaji, na ufuatiliaji wa tathmini ya mazingira. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa kwa sasa kuna Kampuni 138 zenye mikataba katika maeneo ya Hifadhi za Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwepo utaratibu huo Kamati imebaini kuwa kuna mlolongo mrefu wa upatikanaji wa kibali cha kufanya biashara ya utalii na uwekezaji kutokana na kuhusisha mamlaka mbalimbali za Serikali kama vile BRELA, TRA, TIC, NEMC, Uhamiaji na nyinginezo ambao unakwamisha wawekezaji wenye nia ya kuwekeza nchini. Ni rai ya Kamati kuwa ili kupunguza mlolongo huu ni vema Serikali ikaweka mfumo wa dirisha moja (single window) ili kuwezesha wawekezaji kupata leseni kwa urahisi na kwa muda mfupi.

**b) Semina kuhusu Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi.**

**Mheshimiwa Spika**, semina hii ilitolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi kwa lengo la kuwajengea wajumbe uwezo juu ya mradi huu ambapo Kamati ilielezwa kuwa Serikali imepata mkopo kutoka Benki ya Dunia wa **Dola za Kimarekani Milioni 150** sawa na **Shilingi Bilion 375** utakaotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano (2022/2023 hadi Juni, 2027). Aidha, Kamati ilielezwa kuwa mradi huu unalenga kuimarisha usalama wa taarifa za ardhi, kuimarisha miundombinu ya upimaji na kujenga majengo ya Ofisi.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu umegawanyika katika vipengele vinne, kipengele cha kwanza kinahusu kuongeza usalama wa Milki ambapo kitagharimu kiasi cha **Bilioni 167.1** ambazo pamoja na mambo mengine **Bilioni 3**.4 zitatumika kuweka Mpango wa Matumizi ya ardhi kwenye vijiji 250. Kipengele cha pili ni kujenga mifumo ya usimamizi wa ardhi ambao utagharimu kiasi cha **Bilioni 76.9.** kipengele cha tatu kinahusu uratibu wa mradi ambapo utagharimu **Bilioni 55** na kipengele cha nne kitagharimu kiasi cha **Shilingi Bilioni 46.8** ambazo zinalenga kuboresha miundombinu ya usimamizi wa ardhi**.**

**Mheshimiwa Spika**, matarajio ya Wajumbe wa Kamati ni kwamba sehemu kubwa ya fedha ingeelekezwa kwenye mipango ya matumizi ya ardhi ambayo imeonekana kuwa ni suluhisho la migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali nchini hasa wakulima na wafugaji lakin hali halisi inaonyesha kwamba ni **Asilimia 1** tu ya fedha zote ndiyo itaelekezwa kwenye zoezi hilo. Lakini kinyume chake fedha nyingi zimeelekezwa katika kutekeleza mambo mengine kama vile uratibu wa mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haioni tija katika mradi huu kwa kuwa haugusi kwa kiwango cha kutosha maeneo yanayolenga kutatua migogoro ya ardhi nchini. Aidha, utekelezaji wa mradi huu ungeweza kutekelezwa kwa ufanisi endapo wangeiwezesha Tume ya Mipango ya Ardhi ambayo imekuwa ikitekeleza majukumu yake ya upangaji kwa ufanisi; hata hivyo ufinyu wa bajeti umefanya ishindwe kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mathalani hadi kufikia Desemba 2022 ni vijiji 2,678 kati ya vijiji 12,319 vilivyopo nchini ndio vimepangiwa matumizi ya ardhi.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusu shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha kuanzia Februari 2022 hadi Januari 2023 ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati Kamati ikitimiza majukumu yake.

#### 3.1.1 Wizara ya Maliasili na Utalii

i) Serikali kuweka mikakati ya kulinda maeneo yaliyohifadhiwa na kuweka alama za kudumu na zenye kuonekana ili kudhibiti uvamizi wa shughuli za kibinadamu.

ii) Serikali kuongeza Bajeti ya Chuo cha FITI ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

iii) Serikali ichukue hatua madhubuti za kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa uhifadhi ili kunusuru misitu yetu nchini.

iv) Serikali iweke mkakati wa kuvitambua, kuviendeleza na kuvitangaza vivutio vyote vya utalii nchini ikiwa ni pamoja na utalii wa malikale, utalii wa fukwe za bahari, uvuvi, utamaduni na maeneo mengine

v) Serikali ione namna bora ya kuboresha taratibu za manunuzi ili iweze kutatua changamoto zilizopo katika Sekta ya Utalii hasa upatikanaji wa mitambo na magari yanayonunuliwa kupitia GPSA.

vi) Serikali iajiri Askari Uhifadhi wa kutosha ili kuimarisha doria na kukabiliana na ujangili pamoja na kuzuia athari za wanyama wakali na waharibifu.

vii) Serikali iweke mfumo mzuri wa uwekezaji katika sekta ya utalii ili kupunguza mlolongo mrefu wa upatikanaji wa vibali vya uwekezaji.

viii) Serikali ione umuhimu wa kuwatumia Mabalozi wetu katika nchi mbalimbali duniani kutangaza na kuhamasisha utalii ili kuongeza idadi ya watalii na mapato yatokanayo na utalii.

ix) Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Ardhi kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ili kupunguza migogoro baina ya hifadhi na wananchi.

x) Kuweka mikakati ya kuchimba mabwawa na visima vya maji kwa ajili ya wanyamapori kwenye maeneo ambayo yana upungufu wa maji ili kupunguza kasi ya wanyama hao kuvamia maeneo ya makazi ya wananchi kutafuta maji; na

xi) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu maeneo ya shoroba za wanyamapori ili kupunguza muingiliano kwa wanyama na binadamu unaoleta athari kwa pande zote.

### 3.1.2 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

i) Hatua za haraka zichukuliwe kufuta GN zilizoanzisha Mapori Tengefu ya Handeni na Kitwai yaliyopendekezwa kuwa makazi ya wanaohamia kutoka Ngorongoro ili kuziwezesha mamlaka za upangaji kukamilisha kazi yao.

ii) Kutokuwepo kwa mabaraza ya Ardhi na Nyumba kila wilaya nchini kumepelekea baadhi ya wananchi kulazimika kusafiri umbali mrefu kufuatilia mashauri yao, Serikali iharakishe kuanzisha mabaraza haya kila wilaya.

iii) Serikali ibuni mbinu mbalimbali za kuhamasisha wananchi kulipa kodi za ardhi, kama vile kufanya matangazo kwenye mikusanyiko mbalimbali;

iv) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuzingatia mpango wa matumizi ya ardhi sambamba na ushirikishwaji wa wananchi.

## 3.2 MAPENDEKEZO

### 3.2.1 Maboresho ya eneo la hifadhi ya ngorongoro

**KWA KUWA**, Serikali imepiga hatua nzuri katika kuhakikisha kuwa inainusuru Hifadhi ya Ngorongoro ambayo ilikuwa katika hatari ya kutoweka kutokana na ongezeko kubwa la watu na shughuli zao kinyume na lengo la uanzishwaji wake;

**NA KWA KUWA**, zoezi linaloendelea la kuhamisha wakazi wanaoishi ndani ya hifadhi hii kuwapeleka maeneo mengine nje ya hifadhi limeonesha mafanikio makubwa baada ya wakazi wengi kukubali kuhama kwa hiari;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kutekeleza mambo yafuatayo ili kuhakikisha zoezi hili linafanikiwa kwa ufanisi na kwa wakati: -

(i) Kuharakisha kutoa fedha na kwa wakati ili kufanikisha kukamilisha zoezi la kuhamisha wakazi wa Ngorongoro,

(ii) Kuharakisha mchakato wa kufanya marekebisho ya sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kuendana na hali ya sasa

### 3.2.2 Urejeshaji wa Asilimia 30 ya Makusanyo (retention)

**KWA KUWA**, utaratibu wa kubakisha **Asilimia 30** ya makusanyo (retention) kwa wizara ya Maliasili na Utalii kwa ajili ya kurahisishia wizara kutekeleza majukumu yake uliondolewa,

**NA KWA KUWA**, kuondolewa kwa utaratibu huo kumechangia kuathirika kwa kwa kiasi kikubwa kasi ya utekelezaji wa majukumu ya wizara hasa yale yanayohitaji fedha wakati wote kama vile huduma za TEHAMA katika maeneo yanayohitaji *internet*, matukio ya ujangili na majanga ya moto;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri Serikali kuona uwezekano wa kufanya Marekebisho ya Sheria ya Fedha Na.8 /2020 kwa lengo la kurejesha sehemu ya makusanyo(retention) ili kuisaidia wizara kutekeleza majukumu yake hasa yale yanayohitaji fedha muda wote au kuanzisha Mfuko wa Kusaidia Masuala ya Uhifadhi.

### 3.2.3 Kulijengea uwezo Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)

**KWA KUWA**, idadi ya Hifadhi za Taifa imeongezeka kutoka hifadhi 16 hadi 22 ambapo pamoja na kuongezeka bado shirika linatumia bajeti iliyotengwa kuhudumia hifadhi 16 tangu Mwaka 2019 ambazo bado ilikuwa haitoshelezi;

**NA KWA KUWA,** ongezeko la hifadhi 6 limezidi kuiongezea mzigo TANAPA kwa kuwa sehemu za kiutawala zimeongezeka na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kuliongezea bajeti Shirika ili liweze kutekeleza majukumu yake na kuleta tija iliyokusudiwa.

### 3.2.4 Changamoto za Wanyamapori Wakali na Waharibifu

**KWA KUWA**, mgongano baina ya binadamu na wanyamapori ni moja ya changamoto zinazokabili uhifadhi wa wanyamapori nchini;

**NA KWA KUWA**, mgongano huo umeleta athari pande zote kwa uharibifu wa mali, kujeruhi hata kuuwawa kwa binadamu na wanyamapori;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashuri Serikali yafuatayo: **-**

(i) Kuongeza kasi ya ujenzi wa vituo vya udhibiti wa wanyama wakali na waharibifu nchini na uajiri Askari Uhifadhi ili kupunguza athari kwa wananchi;

(ii) Kuweka teknolojia ya kuthibiti wanyama wakali na wahalibifui;

(iii) Kufanya marejeo ya Kanuni za Malipo ya Kifuta Machozi/Jasho ya Mwaka 2001 ili kuboresha viwango kwa aliyeathirika na wanyama wakali na waharibifu ili kuendana na hali maisha ya sasa.

### 3.2.5 Kutungwa kwa Sheria ya Uendeshaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA)

**KWA KUWA**, Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania ilianzishwa kwa amri ya kisheria *(establishment order)* na Waziri mwenye dhamana chini ya Kifungu cha 8 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 ili kusimamia mapori ya akiba, mapori tengefu, jumuiya za hifadhi ya wanyamapori na maeneo ya ardhi oevu ambapo mamlaka hii inasimamiwa na Bodi ya Ushauri badala ya Bodi ya Utendaji;

**NA KWA KUWA**, Hali hii inaathiri utendaji wa mamlaka kwa kuwa inakosa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori itakayoainisha bayana majukumu yake na kuanzisha Bodi ya Utendaji itakayoipa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake.

### 3.2.6 Hali ya Utalii Nchini

**KWA KUWA**, sekta ya utalii ina mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa kwa kuchangia zaidi ya **asilimia 25** ya mauzo yote ya nje kabla ya UVICO – 19;

**NA KWA KUWA,** sekta hii ilianguka kwa kiasi kikubwa kutokana na mlipuko wa janga la UVIKO – 19 ambalo lilisababisha idadi ya watlii kupungua na kuepelekea kushuka kwa mapato;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali yafuatayo: **-**

**(i)** Iweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Rais wa Jmahuri ya Muungano wa Tanzania kupitia program ya *Tanzania- the Royal Tour* inakuwa endelevu kwa kuweka mazingira mazuri yatakayohakikisha watalii wanaendelea kuja na kufurahia utalii Tanzania;

**(ii)** Iweke mkakati wa kutumia mabalozi wetu katika nchi mbalimbali duniani katika kutangaza na kuhamasisha utalii ili kuongeza idadi ya watalii na mapato yatokanayo na utalii; na

### 3.2.7 Changamoto za Taasisi za Utafiti za (TAFORI & TAWIRI)

**KWA KUWA**, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI) zinakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti na changamoto ya muundo katika Taasisi ya TAFORI;

**NA KWA KUWA**, changamoto hizi zinaathiri ufanisi wa taasisi hizo katika kufanya, kusimamia, kuratibu tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika sekta husika;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri kwamba: -

**(i)** Taasisi hizo zipewe kipaumbele na ziongezewe bajeti ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria; na

**(ii)** Serikali iharakishe kuhuisha muundo wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu ili kuwezesha taasisi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi**.**

### 3.2.8 Usimamizi wa Rasilimali za Misitu Nchini

**KWA KUWA,** Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wamekuwa wakifanya kazi nzuri ya udhibiti wa matumizi ya rasilimali za misitu ya Serikali Kuu peke yake na kuziacha rasilimali zingine za misitu zisizo za serikali bila udhibiti madhubuti wa matumizi;

**NA KWA KUWA,** changamoto ya udhibiti wa matumizi ya rasilimali za misitu isiyokuwa ya Serikali pamoja na kuleta mgongano kwenye matumizi ya rasilimali hizo, kunachangia kuleta uharibifu na kutishia uendelevu wa misitu yetu;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linashauri Serikali kwa mara nyingine, kuharakisha kukamilisha mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania ili kuipa nguvu ya kisheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu yote nchini.

### 3.2.9 Kutokuwepo kwa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba kila Wilaya Nchini

**KWA KUWA**, kutokuwepo kwa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya katika kila wilaya nchini kumepelekea baadhi ya wananchi kukosa huduma hiyo kwa karibu na kwa wakati;

**NA KWA KUWA;** kukosekana huko kwa huduma karibu na wananchi kumepelekea wananchi kulazimika kusafiri umbali mrefu kufuatilia mashauri yao

**KWA HIYO BASI;** Bunge linaishauri Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:

(i) Kutenga fedha za kutosha kuanzisha mabaraza ya ardhi kila wilaya na kuajiri watendaji wa mabaraza hayo ili kusogeza huduma karibu na wananchi; na

(ii) Kuwekeza kwenye mabaraza yanayotembea (Mobile Land Tribunal) ili kuwafikia wananchi wengi kwenye kata na vijiji.

### 3.2.10 Taasisi na Mashirika ya Umma kutolipa Kodi ya Pango la Ardhi

**KWA KUWA**, kwa muda mrefu sasa baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yamelimbilikiza madeni ya kodi ya pango la ardhi;

**NA KWA KUWA,** malimbikizo hayo kwa kiasi kikubwa yameathiri makusanyo ya Wizara na kukwamisha baadhi ya shughuli muhimu za sekta ya ardhi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaishauri Serikali kusimamia mikakati yake kwa kuzitaka taasisi zote kulipa malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi.

### 3.2.11 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Mawaziri 8 wa Kisekta katika Kutatua Migogoro ya Vijiji 975 Nchini

**KWA KUWA**, kutokana na kuwepo kwa migogoro ya ardhi nchini Serikali iliunda Kamati ya Mawaziri 8 wa Kisekta ili kuona namna bora ya kutatua migogoro ya ardhi katika vijiji 975 nchini ambapo Kamati hiyo ilipelekea kupatikana kwa mapendekezo ambayo yaliwasilishwa na kukubaliwa na Baraza za Mawaziri;

**NA KWA KUWA**, utekelezaji wa mapendekezo ya Baraza la Mawaziri umekuwa na changamoto kutokana na maeneo yanayotekelezwa mapendekezo hayo kutokuwa shirikishi katika ngazi za chini na kukosekana kwa nyenzo ya ufuatiliaji wa maagizo ya utekelezaji yanayotolewa kwa uongozi wa Mikoa na Wilaya;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali yafuatayo: -

(i) Kuweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha utekelezaji wa mapendekezo haya unakuwa shirikishi ili kuepuka kuanzisha migogoro mipya;

(ii) Maeneo yaliyobadilishiwa matumizi yamewekewe mipaka ya kudumu ili kuepuka kuvamiwa na kuzalisha migogoro mipya; na

(iii) Kuweka utaratibu maalumu (Mechanisms) ya ufuatiliaji wa maagizo yanayotolewa na Kamati ya Mawaziri kwa viongozi wa Mikoa na Wilaya.

(iv) Kamati ya Mawaziri 8 kuendelea kutatua migogoro kwa kufika kwenye maeneo ya migogoro (uwandani) ili kuona uhalisia na kutatua migogoro badala ya kuishia kwenye ofisi za Mkoa na Wilaya.

### 3.2.12 Kuhuisha Sera mbalimbali zilizopitwa na wakati

**KWA KUWA**, Sera nyingi katika sekta ya Ardhi na za Maliasili na Utalii zimepitwa na wakati, kwa mfano Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999, Sera

ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya mwaka 1998, Sera ya Malikale ya mwaka 2008; Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2001.

**NA KWA KUWA**, kupitwa huku na wakati kunasababisha ugumu katika kutekeleza baadhi ya mambo ambayo yanatekelezwa kulingana na mabadiliko ya wakati na mazingira;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuzihuisha sera zilizopitwa na wakati na sheria zinazohitaji maboresho ili kuwezesha utekelezaji wake kuwa na ufanisi

### 3.2.13 Kuanzishwa kwa Mamlaka ya kusimamia Sekta ya Nyumba Nchini (Real Estate Regulatory Authority - RERA)

**KWA KUWA**, nchi yetu haina mamlaka inayosimamia sekta ya nyumba na limekuwa ni tatizo la muda mrefu;

**NA KWA KUWA,** Kukosekana kwa Mamlaka ya kusimamia sekta ya Nyumba (Real Estate Regulation and Control) nchini kumepelekea kuwepo kwa utitiri wa madalali wa nyumba, uholela wa bei za kupanga na hata kuikosesha mapato Serikali kwa kiasi kikubwa;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya kusimamia Sekta ya Nyumba ili kuwepo na chombo madhubuti kinachosimamia sekta ya nyumba nchini.

### 3.2.14 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

**KWA KUWA**, migogoro mingi ya ardhi nchini inasababishwa na ardhi kutokupangiwa matumizi, ambapo hadi sasa ni vijiji 2,678 tu vimepimwa kati ya vijiji 12,319 vyote nchini,

**NA KWA KUWA**, Kasi ndogo ya upangaji inatokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi ambayo imepewa jukumu la kupanga matumizi ya ardhi nchi nzima,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri Serikali yafuatayo: -

(i) Kuhakikisha kuwa, fedha za nyongeza **Shilingi Bilioni 4** zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa kwa wakati ili kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa; na

(ii) Kuendelea kuongeza fedha za maendeleo kwa Tume ili kuhakikisha kila kipande cha ardhi nchini kinapangiwa matumizi na kumaliza migogoro.

**3.2.15 Maboresho ya Mfumo Unganishi wa Kumbukumbu za Taarifa za Ardhi (ILMIS)**

**KWA KUWA,** nia ya Serikali ya kusimika Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi (ILMIS) katika mikoa yote nchini kwa lengo la kutunza kumbukumbu za ardhi ni njema;

**NA KWA KUWA**, maeneo ambayo yameanza kusimikwa mfumo huu yameonesha udhaifu mkubwa katika utekelezaji wake ambapo mfumo unalalamikiwa kwa namna unavyochelewesha kupatikana kwa hati na kuathiri utunzaji wa kumbukumbu;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali yafuatayo: -

(i) Kuboresha mfumo wa ILMIS katika maeneo yanayokwamisha ufanisi katika utekelezaji wake;

(ii) Kuharakisha usambazaji wa Mfumo huu katika Halmashauri zote nchini ili kufanikisha azma ya Serikali ya kutoa hati kwa muda mfupi; na

(iii) Kuongeza idadi ya watumishi wa kada ya TEHAMA kwa ajili ya kutoa huduma ya kiufundi wakati wote pamoja na vitendea kazi

**3.2.16 Utendaji wa Hotel na Loji za Serikali zilizobinafsishwa**.

**KWA KUWA,** Uwekezaji wa Hotel na loji zilizobinafsishwa hauridhishi kutokana na baadhi ya wawekezaji kutozingatia masharti ya mikataba ya mauziano;

**NA KWA KUWA**, kutozingatiwa huko kwa mikataba ya mauziano kumesababisha lengo la kutatua changamoto ya huduma za malazi hususani idadi ya vyumba na vitanda kwa ajili ya watalii kutotimia;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linashauri Serikali yafuatayo: -

(i) Kuchukua hatua za haraka kwa Wawekezaji wa Loji na Hotel ambao wamekiuka masharti ya Mikataba ikiwa ni pamoja na kuharakisha

mchakato wa kuzirejesha Serikalini na kuzitafutia wawekezaji wenye uwezo wa kuzihudumia.

### 3.2.17 Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi

**KWA KUWA,** Serikali ya Tanzania imepata mkopo kutoka Benki ya Dunia wa **Shilingi Bilioni 345** kwa lengo la kuimarisha usalama wa taarifa za ardhi, kuimarisha miundombinu ya upimaji na kujenga majengo ya Ofisi nchini;

**NA KWA KUWA** mpango wa Matumizi ya **Shilingi Bilioni 345** umeonesha kuweka fedha nyingi zaidi katka masuala ambayo hayana tija ya moja kwa moja kwa wananchi ambao ndio walengwa wa mradi huu

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaishauri Serikali kuupitia upya Mpango wa matumizi ya fedha hizo na kufanya maboresho ili kuelekeza fedha nyingi zaidi katika mpango wa matumizi bora ya ardh na kuimarisha mfumo wa ILMISi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO NA KUFUNGA HOJA

### 4.1 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako mafanikio ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kutekeleza Shughuli zake kwa kipindi cha Februari 2022 hadi Januari, 2023 yametokana na juhudi, weledi pamoja na umahiri mkubwa wa Wajumbe katika kushiriki na kutoa maoni yenye tija wakati wote ambapo Kamati imekuwa ikiisimamia Serikali. Ni wazi kwamba, ufanisi wa utendaji wa Kamati hii unatokana zaidi na Ofisi yako kuwajengea uwezo Wabunge na kuwapa msaada stahiki wa kitaalam, na kiushauri wakati wote. Kwa heshima kubwa ningependa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Ally Juma Makoa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Shabani Omary Shekilindi, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Jafari W. Chege, Mb Mjumbe
4. Mhe. Soud Mohamed Juma, Mb ”
5. Mhe. Phillipo Augustino Mulugo, Mb ’’
6. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb ’’
7. Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb ’’
8. Mhe. Neema William Mgaya, Mb ’’
9. Mhe. Asya Mwadini Mohamed, Mb ’’
10. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb ’’
11. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb ’’
12. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb ’’
13. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb ’’
14. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb ’’
15. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb ’’
16. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb ’’
17. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb ’’
18. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb ’’

19. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb ’’
20. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb ’’
21. Mhe. Dkt Florence G. Samizi, Mb ’’
22. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb ’’
23. Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi, Mb ’’
24. Mhe. Mwanakhamis Kassim Said, Mb ’’
25. Mhe. Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mb ’’
26. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb ’’

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Dkt. Angeline S. Mabula (Mb), na Naibu wake Mhe. Ridhiwani J. Kikwete, (Mb) Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dkt. Pindi H. Chana (Mb) na Naibu wake Mhe. Mary F. Masanja, (Mb) Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nimshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote. Vilevile, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Michael Chikokoto, *ndc* pamoja na Makatibu walioandaa taarifa hii akiwemo, Ndg. Ramadhan Abdallah, Ndg. Elieka Saanya na Ndg. Rehema Kipera pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John.

## 4.2 HOJA

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji shughuli hizo, na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Ally Juma Makoa, Mb

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA**

**BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

Februari, 2023